

SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

BARAZA LA MITIHANI LA ZANZIBAR

MTIHANI WA KUINGILIA KIDATO CHA KWANZA

110

SAYANSI JAMII

MUDA: SAA 2:30

JUMATATU 30 OKTOBA, 2023 ASUBUHI

MAELEKEZO KWA MTAHINIWA

1. Mtihani huu una sehemu NNE (4) A, B, C na D.
2. Jibu Maswali YOTE katika sehemu A, B na C. Jibu Maswali MANNE (4) kutoka sehemu D.
3. Andika nambari yako ya mtihani katika kila ukurasa.
4. Majibu yote yaandikwe katika nafasi zilizowekwa.
5. Majibu yote yaandikwe kwa kalamu ya buluu au nyeusi.
6. Simu za mkononi na vitu visivyoruhusiwa havitakiwi ndani ya chumba cha mtihani.

KWA MATUMIZI YA WASAHIHISHAJI		
NAMBARI YA SWALI	ALAMA	SAINI
1.		
2.		
3.		
4.		
5.		
6.		
7.		
8.		
9.		
10.		
11.		
12.		
JUMLA		
SAINI YA MHAKIKI		



023110701

Mtihani huu una kurasa 16 zenye maandishi

Ukurasa wa 1 kati ya 16

SEHEMU A: (Alama 20)

Jibu Maswali YOTE katika sehemu hii.

1. Chagua jawabu sahihi katika vipengele ulivyopewa kisha andika herufi yake kwenye jadwali lililopo hapo chini.
 - i. Tanzania inafuata mfumo wa vyama vingi vya siasa. Ni mwaka gani Tanzania iliingia katika mfumo huo wa siasa?
 - A. 1990
 - B. 1992
 - C. 1995
 - D. 1999
 - ii. Ni miaka ishirini na moja (21) hivi sasa tokea kuanzishwa kwa Umoja wa Africa (AU). Umoja huo ulianzishwa rasmi mwaka gani?
 - A. 2000
 - B. 2001
 - C. 2002
 - D. 2003
 - iii. Wafuatao ni viongozi wa Baraza la Mawaziri la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania **isipokuwa**
 - A. Raisi wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania
 - B. Raisi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar
 - C. Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar
 - D. Waziri Mkuu wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania
 - iv. Kati ya njia zifuatazo, ni njia ipi haihusiani na utoaji wa taarifa za tahadhari?
 - A. Filimbi na mayowe
 - B. Kukimbia na kilio
 - C. Kukimbia na kucheka
 - D. Simu na kilio

- v. Moja kati ya malengo ya kuanzishwa Umoja wa Afrika (AU) ni kulinda uhuru na utawala wa
- A. India
 - B. Nchi wanachama
 - C. Nchi za Ulaya
 - D. Zanzibar
- vi. Ifuatayo ni misingi mikuu inayopatikana katika Katiba ya Zanzibar **isipokuwa**
- A. Kuwepo uhuru wa mahakama
 - B. Mashirikiano baina ya vyombo vya dola na jamii
 - C. Mgawanyo wa madaraka
 - D. Usawa mbele ya sheria
- vii. Lugha ambayo huunganisha nchi za Jumuiya ya Madola ni
- A. Kifaransa
 - B. Kiingereza
 - C. Kijerumani
 - D. Kiswahili
- viii. Miongoni mwa maelezo yafuatayo, ni yepi yanaeleza maana sahihi ya jinsia?
- A. Hali ya maumbile kwa mwanamke au mwanaume
 - B. Hali ya maumbile ya wazazi na watoto
 - C. Mahusiano kati ya familia moja na nyengine
 - D. Mahusiano ya kijamii kati ya mwanamke na mwanaume
- ix. Ni ipi kati ya haki za binadamu zifuatazo inapakitaka katika haki za kizazi cha kwanza?
- A. Kufanya kazi
 - B. Kupata elimu
 - C. Kupata maendeleo
 - D. Uhuru wa mawazo

- x. Miongoni mwa madhara ya rushwa katika jamii ni
- A. Kupata huduma kwa haraka zaidi
 - B. Kupata maslahi mazuri kwa mfanyakazi
 - C. Kupatikana kwa maslahi binafsi
 - D. Kupatikana kwa usalama wa raia

JAWABU

i.	ii.	iii.	iv.	v.	vi.	vii.	viii.	ix.	x.

2. Andika **Kweli** kwa maelezo yaliyo sahihi au **Si kweli** kwa maelezo yasiyo sahihi katika jadwali lililopo hapo chini.

- i. Katiba ya kwanza ya Zanzibar iliandikwa mwaka 1984.
- ii. Utawala bora huzingatia haki za binadamu na utawala wa sheria.
- iii. Raisi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ana mamlaka ya kuvunja Bunge.
- iv. Mtu anapopata maradhi ya UKIMWI anatakiwa ajitenge na jamii yake.
- v. Mfumo wa vyama vingi vya siasa ni mfumo wenye gharama kubwa.
- vi. Matumizi ya dawa za kulevya humuathiri mtumiaji na familia yake.
- vii. Spika wa Bunge ndiye kiongozi wa shughuli za serikali Bungeni.
- viii. Moja kati ya kazi za JKU ni kuzuwia magendo.
- ix. Jumuiya ya Africa ya Mashariki inajihusisha na uhifadhi wa mazingira.
- x. Umoja wa Mataifa ulianzishwa rasmi tarehe 25/9/1945.

JAWABU

i.	ii.	iii.	iv.	v.	vi.	vii.	viii.	ix.	x.

SEHEMU B: (Alama20)

Jibu Maswali YOTE katika sehemu hii.

3. Jaza nafasi zilizowazi kwa kuandika jibu sahihi ulilopewa kwenye sanduku.

Ufaransa, Kenya, serikali ya kikoloni, Shirazi Association, Ujerumani, Uganda, African Youth Union, kukosekana uwazi katika nchi, 1844, African Association, Wamishionari, kudumaa kwa demokrasia, 1887, wakunga wa jadi

- a) Chama cha Afro - Shirazi (ASP) kilianzishwa mwaka 1957 kwa kushirikisha Viongozi wa _____ na _____
- b) Huduma za afya wakati wa ukoloni zilitolewa na _____ wakisaidiana na _____
- c) Mfano wa nchi iliyotumia mfumo wa utawala wa moja kwa moja wakati wa ukoloni Africa mashariki ni _____ wakati mfano wa nchi iliyotumia mfumo usio wa moja kwa moja ni _____
- d) Miongoni mwa athari hasi za mfumo wa chama kimoja ni _____ na _____
- e) Ludwig Krapf ni miongoni mwa Wamishionari kutoka _____ aliyekuja Afrika kuhubiri amani na upendo. Mmishionari huyo alikuja Zanzibar mwaka _____

4. Oanisha maelezo yatokanayo na mfumo wa Umwinyi kutoka **KIFUNGU A** na maneno sahihi kutoka **KIFUNGU B**. Andika herufi ya jawabu katika jadweli lililopo hapo chini.

KIFUNGU A	KIFUNGU B
i. Aliteuliwa kukusanya kodi kutoka kwa wakulima	a. Diwani
ii. Walikuwa wakikodi ardhi kutoka kwa Mamwinyi kwa shughuli za kilimo	b. Nokoa
iii. Aliteuliwa kumsaidia Mwinyi Mkuu kwa upande wa Unguja	c. Omukama
iv. Ni mfumo ambao watu wachache humiliki mali kwa manufaa yao binafsi	d. Sebuja
v. Aliteuliwa kumsaidia Mwinyi Mkuu kwa upande wa Pemba	e. Shakua
	f. Sheha
	g. Umwinyi
	h. Watwana

JAWABU

KIFUNGU A	i.	ii.	iii.	iv.	v.
KIFUNGU B					

SEHEMU C: (Alama 20)

Jibu maswali YOTE katika sehemu hii.

5. Jibu kwa ufupi maswali yafuatayo.
- a) Bainisha faida mbili (2) za msitu wa mkoko kwa jamii ya Zanzibar.

- i. _____

- ii. _____

b) Chora alama inayoonesha vitu vifuatavyo katika ramani:

i. Daraja

ii. Nyumba

c) "Visiwa vya Zanzibar huwa na hali ya hewa ya joto kwa muda wa mwaka mzima". Kwa kutumia hoja mbili (2) eleza kwa ufupi sababu zinazopelekea hali hiyo.

- i. _____


- ii. _____

d) Nini maana ya sensa ya watu?

e) Taja vyanzo viwili (2) vya maji ambavyo tunavitumia katika maisha yetu ya kila siku.

- i. _____
- ii. _____

6. Chunguza kwa makini mchoro uliopo chini kisha jibu maswali yafuatayo:



- a) Taja majina ya mistari ya latitudo iliyowasilishwa kwa herufi zifuatazo:
A: _____
C: _____
- b) Taja mabara mawili (2) ambayo yamepitiwa na mstari wa **B** kwenye mchoro wa hapo juu.
 i. _____
 ii. _____
- c) Andika milima mikubwa miwili (2) iliyopo katika bara liliwasilishwa kwa herufi **M**.
 i. _____
 ii. _____
- d) Taja majina ya bahari mbili (2) zilizozunguka bara lililowasilishwa kwa herufi **O**.
 i. _____
 ii. _____
- e) Bainisha athari mbili (2) za mzunguko wa dunia wa masaa 24 (rotation).
 i. _____
 ii. _____

SEHEMU D: (Alama 40)

Jibu maswali MANNE (4) katika sehemu hii.

7. "Mfumo wa vyama vingi vya siasa una faida na hasara zake katika jamii."
Thibitisha kauli hiyo kwa kueleza faida mbili (2) na hasara mbili (2) za mfumo huo.
8. Fafanua kazi nne (4) za Serikali ya Wilaya.
9. Eleza sababu nne (4) zilizopelekea kuundwa kwa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.
10. Mara baada ya uhuru, nchi za Afrika zilifanya mabadiliko ya utoaji wa huduma katika sekta afya. Chambua mabadiliko manne (4) yaliyojitokeza katika sekta hiyo.
11. "Sekta ya utalii inaleta faida nyingi kwa Taifa". Kwa kutumia hoja nne (4) fafanua dai hilo kwa kuonesha vipi Zanzibar inanufaika na sekta hiyo.
12. Matokeo ya sensa ya mwaka 2022 yanaonesha kuwa, idadi ya watu Tanzania inaongezeka kwa kasi. Kwa kutumia hoja nne (4) eleza jinsi hali hiyo inavyosababisha uharibifu wa mazingira nchini.

Nambari ya Mtahiniwa _____

[illegible]

Nambari ya Mtahiniwa _____

[illegible]

Nambari ya Mtahiniwa _____

[illegible]

Nambari ya Mtahiniwa _____

This image shows a full page of white paper with horizontal blue ruling lines. The lines are evenly spaced and run across the width of the page, providing a template for handwriting practice or general writing. There are no margins, text, or other markings on the page.

Nambari ya Mtahiniwa _____

[illegible]

Nambari ya Mtahiniwa _____

[illegible]

Nambari ya Mtahiniwa _____

[illegible]